

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA  
MTIHANI WA KUHITIMU KIDATO CHA NNE

021

KISWAHLI

(Kwa watahiniwa Walioko na Wasiokuwa Shulen)

Mwaka : 2022

Muda: Saa 3

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C zenyе jumla ya maswali **kumi na mbili (12)**.
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu A na B na maswali **matatu (3)** kutoka sehemu C.
3. Sehemu A ina alama **kumi na tano (15)**, sehemu B alama **arobaini (40)** na sehemu C ina alama **arobaini na tano (45)**.
4. Zingatia maelekezo ya **kila sehemu** na ya **kila swalii**.
5. Simu za mkononi na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** katika chumba cha mtihani.
6. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.



## SEHEMU A (Alama 15)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Chagua herufi ya jibu sahihi katika vipengele (i) hadi (x), kisha andika herufi ya jibu hilo kwenye kijitabu chako cha kujibia.
- (i) “Kushindana na mtu aliyekuzidi kwa kila hali si busara.” Methali zifuatazo zinashabihisha kauli hii **isipokuwa**:
- |                              |                            |
|------------------------------|----------------------------|
| A Mwenye pesa si mwenzio     | B Nazi haishindani na jiwe |
| C Chanda chema, huvikwa pete | D Mwenye nguvu mpishe      |
| E Maji yakija kasi yapishe.  |                            |
- (ii) Neno linaloingizwa katika kamusi kwa wino uliokolezwa, fasili, matamshi na aina ya neno hilo kwa pamoja huitwaje?
- |            |             |
|------------|-------------|
| A Kidahizo | B Kategoria |
| C Fasili   | D Istilahi  |
| E Kitomeo. |             |
- (iii) Kikundi cha maneno kinachoonesha jambo lililotendwa na mtenda katika sentensi hujulikanaje?
- |             |              |
|-------------|--------------|
| A Chagizo   | B Kitenzi    |
| C Kivumishi | D Shamirisho |
| E Nomino.   |              |
- (iv) Bainisha sentensi yenyе vielezi zaidi ya kimoja katika sentensi zifuatazo:
- |   |
|---|
| A Vitabu vyangu vyote vimeibiwa na watoto wako. |
| B Mbuzi aliyepotea jana ameonekana leo asubuhi. |
| C Shule ngapi zinaweza kushiriki mashindano?    |
| D Wengi walikuwa wanataka kwenda masomoni.      |
| E Wanakijiji hawa wamefanya uchaguzi kwa amani. |
- (v) Pande mbili zinazohusika katika lugha ya maandishi ni zippi?
- |                            |                          |
|----------------------------|--------------------------|
| A Mwandishi na msikilizaji | B Msikilizaji na msomaji |
| C Mwandishi na mzungumzaji | D Msomaji na msimulaiji  |
| E Msomaji na mwandishi.    |                          |
- (vi) Dhima ya vigegele katika utendekaji wa sanaa za maonesho ni ipi?
- |  |
|--|
| A Kuishirikisha na kuiondolea hadhira udhia wa kumsikiliza mtu mmoja.  |
| B Hadhira kukata shauri juu ya mwendo wa kazi ya sanaa za maonesho.    |
| C Kuweka alama za mapigo ya kimuziki katika kazi ya sanaa za maonesho. |
| D Kuonesha upeo wa furaha na burudani ya kazi ya sanaa za maonesho.    |
| E Kuonesha mbwembwe katika kazi ya sanaa za maonesho.                  |

- (vii) Njia ipi hutunza sauti pamoja na vidokezo vyake katika kuhifadhi kazi ya fasihi simulizi kati ya hizi?
- A Maandishi
  - B Mikanda ya filamu
  - C Mitandao
  - D Kinasa sauti
  - E Masimulizi.
- (viii) Jambo gani muhimu huzingatiwa na mtunzi wa insha ya hoja?
- A Lugha yenye ukinzani
  - B Lugha isiyo na mvuto
  - C Lugha ya kisanaa
  - D Lugha ya kufikirisha
  - E Lugha inayosifia.
- (ix) Zifuatazo ni kazi za alama ya uandishi *nuktamkato* (;) **isipokuwa:**
- A Kuonesha kwamba vitu vinavyofuata viko katika orodha.
  - B Kuunga mawazo mawili tofauti katika sentensi.
  - C Kuonesha kwamba kinachofuata ni ufanuzi zaidi.
  - D Kuunga mawazo mawili au zaidi katika sentensi.
  - E Kutenga vifungu vya sentensi ambazo ni ndefu.
- (x) Kipi ni kipengele kinachohusu mjengeko wa kazi za fasihi?
- A Mtindo
  - B Muundo
  - C Mandhari
  - D Wahusika
  - E Lugha.

2. Oanisha maana za tamathali za semi zilizo katika **Orodha A** na tamathali husika kutoka **Orodha B**, kisha andika herufi ya jibu sahihi katika kijitabu chako cha kujibia.

<b>Orodha A</b>	<b>Orodha B</b>
(i) Ushangaaji wa jambo fulani, aghalabu huambatana na alama ya mshangao.	A Tashbiha
(ii) Upangiliaji wa maneno katika namna ya kipingana ili kusisitiza mawazo fulani.	B Takrirri
(iii) Ulinganishaji wa vitu viwili au zaidi vyenye sifa tofauti kwa kutumia viunganishi.	C Sitiari
(iv) Uhuishwaji wa kitu kisicho binadamu kupewa uwezo wa kutenda kama binadamu.	D Tabaini
(v) Urudiaji wa meno, herufi au silabi ili kusisitiza jambo.	E Tashihisi
	F Nidaa
	G Tanakali sauti

## SEHEMU B (Alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

3. Kwa kutumia mfano kwa kila moja, fafanua taarifa nne za kisarufi zilizopo katika viambishi awali vyta vitenzi nya Kiswahili.
4. "Fasihi simulizi ni hai." Thibitisha kauli hii kwa kutoa hoja nne na mifano halisi.
5. (a) Kwa kutumia mfano mmoja kwa kila muundo, bainisha miundo minne ya kirai nomino.  
(b) Changanua sentensi zifuatazo kwa njia ya jedwali:
  - (i) Umma unalalamika sana.
  - (ii) Simba ni mkali ila chui ndiye zaidi.
6. Wanafunzi wengi wa Kidato cha Kwanza huchanganya maana za tanzu na vipera nya fasihi simulizi. Ili kuwaondolea mkanganyiko huo, onesha **tofauti** iliyopo kwa kila seti (a) – (d) kwa kutoa maelezo mafupi na mfano kwa kila moja.
  - (a) Ushairi na Mashairi
  - (b) Maigizo na Vichekesho
  - (c) Semi na Misemo
  - (d) Hadithi na Visasili
7. Ukiwa kama Afisa Utalii katika eneo lako, pendekeza namna utakavyokuza na kueneza lugha ya Kiswahili kwa wageni katika vipengele (i) hadi (iv) na kutoa mfano kwa kila moja.
  - (i) Biashara
  - (ii) Utawala
  - (iii) Utamaduni
  - (iv) Mafunzo
8. Soma kifungu cha habari kifuatacho kisha jibu maswali yanayofuata:

Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEKNOHAMA) hutumiwa kwa lengo la kurahisisha utendaji kazi; kuimarisha ufundishaji; uwazi na kuongeza ufanisi. TEKNOHAMA imetambuliwa na wataalamu wa elimu kuwa ni muhimu katika shughuli za ufundishaji na ujifunzaji. Lengo la kutumia TEKNOHAMA ni kurahisisha ufundishaji kwa sababu hudhihirishwa katika hali halisi kwa kutumia aina mbalimbali za TEKNOHAMA.

Dunia ya sasa imebadilika; na mambo ya kijamii na kiuchumi yanategemea sana mitandao ya kompyuta. Katika kipindi cha miongo mitano iliyopita mpaka sasa, matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano yamezidi kuenea katika elimu kote ulimwenguni.

Ili kufanikisha ufundishaji wa mada mbalimbali, mwalimu anahitaji kutumia TEKNOHAMA kwa ajili ya kupata taarifa na habari kutoka vyanzo mbalimbali, kuendeleza ujifunzaji unaompa mwanafunzi nafasi ya kati na kumpa mwalimu jukumu la kuwa mlezi na mwenezi badala ya ule wa mjua vyote. Mwalimu wa karne hii anaweza kujihusisha na matumizi ya TEKNOHAMA katika ufundishaji wake darasani, hali inayoweza kumpa ahueni katika kazi yake.

Hata hivyo, katika nchi zinazoendelea walimu wengi hawatumii TEKNOHAMA katika ufundishaji. Hii inatokana na teknolojia hii kuhitaji muda, fedha na maarifa ya ziada kwa watumiaji. Hayo kwa jumla yanakwamisha utumiaji wa teknolojia hiyo katika elimu. Hivyo hatuna budi kuhakikisha tunakabiliana na mambo hayo ili kuhakikisha teknolojia hiyo inatumika katika elimu ili kurahisisha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.

### Maswali

- (a) Bainisha matumizi manne ya TEKNOHAMA katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji kulingana na habari uliyosoma.
- (b) Fupisha habari hiyo kwa maneno yasiyopungua 60 na yasiyozidi 70.

### SEHEMU C (Alama 45)

Jibu maswali **matatu (3)** kutoka katika sehemu hii.

9. Chama cha Waandishi wa Vitabu Tanzania kimeanzisha shindano la uandishi wa insha kuhusu Manufaa ya Sayansi na Teknolojia kwa Maendeleo ya Kiswahili. Ukiwa mionganini mwa wanachama, andika insha isiyopungua maneno mia mbili (200) na isiyozidi maneno mia mbili hamsini (250) kuhusu shindano hilo.

### ORODHA YA VITABU

#### USHAIRI

Wasakatonge

Malenga Wapya

Mashairi ya Chekacheka

- M.S. Khatibu (DUP)

- TAKILUKI (DUP)

- T.A. Mvungi (EP & D. LTD)

#### RIWAYA

Takadini

Watoto wa Mama N'tilie

Joka la Mdimu

- Ben J. Hanson (MBS)

- E. Mbogo (H.P)

- A.J. Safari (H.P)

#### TAMTHILIYA

Orodha

Ngoswe Penzi Kitovu cha Uzembe

- Steve Reynolds (MA)

- E. Semzaba (ESC)

- Medical Aid Foundation (TPH)

Kilio Chetu

10. Umeagizwa na mwalimu wako wa somo la Kiswahili kutunga shairi moja utakaloghani siku ya mahafali yenu ya kuhitimoo Kidato cha Nne. Lengo la shairi hilo ni kuwasaidia wahitimoo kuboresha maisha yao ya baadaye. Chagua mashairi matatu kwa kila diwani kutoka katika diwani mbili ulizosoma kisha eleza mafunzo utakayoyajumuisha katika shairi lako.
11. "Matatizo ya mwanajamii huletwaa na mwanajamii mwenyewe." Thibitisha usemi huu kwa kutoa hoja tatu kwa kila riwaya kati ya riwaya mbili ulizosoma.
12. "Ujinga ni chanzo cha maendeleo duni katika jamii." Kwa kutumia wahusika watatu kwa kila tamthiliya, onesha jinsi ujinga wao ulivyozorotesha maendeleo katika jamii zao kuitia tamthiliya mbili ulizosoma.